

Maswali

1. Mbona Yusufu aliwekwa gerezani?
2. Nani alilinda Yusufu gerezani?
3. Yusufu alikuwa rafiki wa nani gerezani?
4. Mnyweshaji aliota nini?
5. Mwokaji aliota nini?
6. Nani aliwambia maana ya ndoto zao?
7. Ndoto ya mnyweshaji ilimaanisha nini?
8. Ndoto ya mwokaji ilimaanisha nini?
9. Ndoto zilithibitishwa namna gani?
10. Nini ilifanyika kwa Yusufu?

Majibu

1. Mke wa Potifa alisema uongo juu ya Yusufu.
2. Mungu alilinda Yusufu alipokuwa gerezani.
3. Yusufu alikuwa rafiki wa mnyweshaji mkuu wa Farao na mwokaji mkuu.
4. Mnyweshaji aliota juu ya mzabibu wa matawi 3. Ulichipuka, ukatoa maua na kuweka mizabibu. Alizikamua ndani ya kikombe cha Farao.
5. Mwokaji aliota kwamba alikuwa na vikapu 3 vya mikate juu ya kichwa chake. Ndege walitua juu kwa vikapu wakila hizo mikate.
6. Yusufu aliuliza Mungu ndiyo akawambia tafsiri ya ndoto zao.
7. Mnyweshaji atakuwa mnyweshaji tena baada ya siku 3.
8. Mwokaji atanyongwa baada ya siku 3 na ndege watakula mwili wake.
9. Baada ya siku 3 ilikuwa siku kuu ya Farao kuzaliwa. Alirudishia mnyweshaji kazi yake na akanyonga mwokaji.
10. Yusufu alizahauliwa na mnyweshaji. Alibaki gerezani kwa miaka mingine miwili.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



12 Yusufu gerezani

Kwa Biblia Mwanzo 39 na 40

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yusufu aliamini Mungu hata wakati alikuwa gerezani. Mungu alitimiza kuzudi lake kupitia kwa maisha ya Yusufu.

Somo

Yusufu alifurahi kumfanyia Potifa kazi. Alikuwa bwana wa huruma na mzuri. Yusufu alipotamani kwao, alikumbuka kwamba Mungu ako karibu naye kila wakati. Yusufu alifarijika kwa sababu alijua kwamba Mungu alikuwa akimlinda.

Potifa alikuwa na mke muovu. Alijaribu kumshawishi Yusufu afanyie Potifa makosa kwa kumdanganya. Lakini Yusufu alikataa kufanya makosa. Mke wa Potifa alikasirikia Yusufu. Akasema uongo kwa Potifa kumhusu Yusufu. Potifa aliamini uongo alioambiwa na mkewe. Alikasirika kwa sababu alifikiri Yusufu alimdanganya na akafanya hayo makosa. Potifa aliamrisha Yusufu atupwe gerezani.

Mara tena Yusufu akawa na upweke na huzuni. Mara tena akapelekwa mbali na makao yake na kwa rafiki zake. Lakini katika huzuni wake alimpenda na kutii Mungu.

Yusufu alijua kwamba ni lazima Mungu ana sababu ya kukubali haya yote yamfanyikie. Mungu alimsaidia Yusufu na kumbariki. Huko gerezani, mlinzi wa gereza alifanya Yusufu asimamie wafungwa wengine.

Yusufu alikuwa rafiki wa wafungwa wawili gerezani. Walikuwa mnyweshaji mkuu na mwokaji mkuu wa Farao. Walimkosea Farao na akawatupa gerezani. Usiku mmoja mnyweshaji na mwokaji waliota ndoto. Waliota kwamba walikuwa wanamtumikia Farao tena. Walipoamka asubuhi walijikuta wangali gerezani, wakajihurumia sana. Walifadhaika kwa sababu hawakujua maana ya hizo ndoto.

Yusufu aliuliza mnyweshaji na mwokaji mbona walijihurumisha. Walimwambia Yusufu ndoto zao. Yusufu aliwambia kwamba atauliza Mungu amwambie maana ya hizo ndoto. Mungu alifurahi kwa kuona Yusufu anampenda na kumwamini. Alionyesha Yusufu maana ya hizo ya ndoto.



Mnyweshaji mkuu aliota kwamba aliona mzabibu na matawi matatu. Akaona hayo matawi yanachipua maua. Akaangalia zabibu zikakua na kuiva. Mnyweshaji akazichukua hizo zabibu na kuzikamulia kwa kikombe cha Farao. Akampelekea Farao ili anywe.



Yusufu aliambia mnyweshaji kwamba matawi matatu ina maana ya siku tatu. Baada ya siku tatu, Farao atamtoa gerezani na kumfanya mnyweshaji tena. Yusufu akamwambia mnyweshaji amkumbuke wakati atakuwa akimhudumia Farao tena. Alimwambia mnyweshaji aambie Farao amtoe gerezani kwa sababu hakufanya kosa lolote.

Mnyweshaji mkuu alifurahi sana aliposikia tafsiri ya ndoto yake. Mwokaji mkuu alikuwa na tumaini kwamba ndoto yake pia itakuwa na tafsiri nzuri. Aliambia Yusufu kuhuzu ndoto yake.

Mwokaji mkuu aliota kwamba alikuwa amebeba vikapu vitatu vyeupe kichwani. Vikapu vilijaa mikate na alikuwa anapelekea Farao. Njiani ndege walipaa, wakatua juu ya kikapu wakikula hizo mikate.

Yusufu hakukuwa na furaha alipokuwa akimwambia mwokaji tafsiri ya ndoto yake. “Baada ya siku tatu Farao atakutoa gerezani. Lakini utanyongwa ufe na ndege watakukula.



Ilitokea vile Mungu alikuwa ameonyesha kwa ndoto. Baada ya siku tatu ilikuwa siku kuu ya kuzaliwa kwa Farao. Kulikuwa na karamu kubwa. Farao alisamehe mnyweshaji mkuu. Alimtoa gerezani na kumrudishia kazi yake ya mnyweshaji mkuu. Lakini mwokaji mkuu alinyongwa.

Yusufu alingojea mnyweshaji ambie Farao amtoe gerezani. Alingoja kila siku aajiliwe. Lakini mnyweshaji alisahau maneno ya Yusufu. Kwa hivyo Yusufu alikaa gerezani miaka mingine miwili. Lakini Mungu hakukuwa amemsahau Yusufu. Tutasoma vile Yusufu alitoka gerezani kwa somo litakalofuata.